10

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI ZANZIBAR, OKTOBA, MWAKA 2025

14 Novemba 2025

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## Utangulizi

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili; ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa Maeneo ya Utawala, kijiografia, na kijinsia.

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirikana hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi mbali mbali.


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumika na wapangaji, watunga sera, watoa maamuzi na wasimamizi wa sheria.

## Ajali za Barabarani

Jumla ya ajali 31 zimeripotiwa mwezi Oktoba, 2025. Wilaya ya Kati imeripotiwa kuwa na ajali nyingi, ajali sita (6) sawa na asilimia 19.4 ukilinganisha na wilaya nyingine.


**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Oktoba 2025**




Idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Oktoba, 2025 zilikuwa idadi sawa na ajali zilizoripotiwa mwezi Septemba 2025 (ajali 31 kwa kila mwezi).

Mwezi wa Oktoba 2025, Wilaya ya Kati imeripotiwa kuwa na ajali zaidi, ajali sita (6) ikilinganishwa na mwezi wa Septemba 2025 ambapo wilaya ya Magharibi 'B'' iliripotiwa kuwa na ajali zaidi, ajali tano (5).


**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwezi wa Oktoba 2025 na Septemba 2025**



Idadi ya Ajali za barabarani kwa mwaka zimeongezeka kwa asilimia 63.2 na kufikia ajali 31 kwa mwezi wa Oktoba 2025 ikilinganishwa na ajali 19 zilizoripotiwa mwezi wa Oktoba 2024


Wilaya ya Kati imeripotiwa kuwa na ajali zaidi kwa mwezi wa Oktoba 2025 (ajali 6) na Wilaya ya Kaskazini 'A' iliripotiwa kuwa na ajali zaidi mwezi Oktoba 2024 (ajali 8).

**Kielelezo 1.3: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani Kwa Mwezi wa Oktoba 2025 na Oktoba 2024**




Jumla ya waathirika 51 wameripotiwa mwezi Oktoba, 2025 ambapo waathirika 43 walikuwa wanaume na waathirika nane (8) walikuwa wanawake. Wilaya ya Wete imeripotiwa kuwa na waathirika wengi, waathirika 11 sawa na asilimia 21.6 ikilinganishwa na wilaya nyengine.


**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Oktoba 2025**




Idadi ya waathirika waliofariki mwezi Oktoba 2025 imeongezeka kwa asilimia 52.4 na kufikia waathirika 32 kutoka waathirika 21 kwa mwezi wa Septemba 2025.


Idadi ya juu ya waathirika waliofariki kwa mwezi wa Oktoba 2025 wameripotiwa kutoka Wilaya ya Kaskazini 'A' na Magharibi 'A' waathirika sita (6) kwa kila wilaya ikilinganishwa na mwezi wa Septemba 2025 waliripotiwa waathirika wanne (4) kwa kila wilaya kutoka wilaya ya Kati na Kusini.

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Oktoba 2025 na Septemba 2025**




Waathirika waliojeruhiwa mwezi Oktoba 2025 wamepungua kwa asilimia 24.0 na kufikia waathirika 19 kutoka waathirika 25 mwezi Septemba 2025, aidha, kwa mwezi Oktoba 2025 wilaya ya Wete ilikuwa na idadi kubwa ya waathirika waliojeruhiwa (waathirika 8) na Mwezi Septemba 2025 idadi kubwa ya waathirika waliojeruhiwa walitoka wilaya ya Kaskazini 'B' (waathirika 10)

**Kielelezo 1.6: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi Oktoba 2025 na Septemba 2025**





Waathirika waliofariki mwezi wa Oktoba 2025 wameongezeka na kufikia waathirika 32 kutoka waathirika 16 waliofariki mwezi wa Oktoba 2024. Idadi kubwa ya waathirika waliofariki kwa mwezi Oktoba 2025 wameripotiwa kutoka Wilaya ya Kaskazini 'A' na Magharibi 'A' (waathirika sita (6) kwa kila wilaya) ikilinganishwa na mwezi Oktoba 2024 ambapo Wilaya ya Kaskazini 'A' na Magharibi 'B' ziliripotiwa kuwa na waathirika wanne (4) kwa kila wilaya.

**Kielelezo 1.7: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Oktoba 2025 na Oktoba 2024**





Waathirika waliojeruhiwa mwezi wa Oktoba 2025 wamepungua kwa asilimia 5.0 na kufikia waathirika 19 kutoka waathirika 20 walijeruhiwa kwa mwezi Oktoba 2024. Wilaya ya Wete imeripotiwa kuwa na waathirika wengi waliojeruhiwa kwa mwezi wa Oktoba 2025 (waathirika 8) na Wilaya ya Kaskazini 'A' imeripotiwa kuwa na waathirika wengi waliojeruhiwa mwezi Oktoba 2024 (waathirika 16).

**Kielelezo 1.8: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Oktoba 2025 na Oktoba 2024**




Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani waliojeruhiwa na waliofariki mwezi Oktoba 2025, waathirika wengi walikuwa ni abiria 22, wakifuatiwa na wapanda baskeli na pikipiki 18, waendao kwa miguu nane (8) na madereva watatu (3).

**Kielelezo 1.9: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Oktoba 2025**





Ajali nyingi zilizoripotiwa mwezi Oktoba 2025 zilitokea muda wa saa 12:01 jioni hadi 03:00 usiku ambapo zimeripotiwa ajali 8.

**Kielelezo 1.10: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Oktoba 2025**




Kati ya ajali 31 zilizoripotiwa mwezi wa Oktoba 2025, ajali 25 zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali sita (6) zimesababishwa na uzembe wa madereva. Mkoa wa Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Mjini Magharibi ina idadi kubwa ya ajali zilizosababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi (ajali 7) kwa kila mkoa. Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya ajali zilizosababishwa na uzembe wa madereva (ajali 2).

**Kielelezo 1.11: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa, Oktoba 2025.**




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 5,631 yameripotiwa mwezi wa Oktoba 2025, ambapo makosa 5,629 yameripotiwa kwa wanaume na makosa mawili (2) yameripotiwa kwa wanawake.

Wilaya ya Mjini ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani ,makosa 1,262 sawa na asilimia 22.4 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa kwa mwezi Oktoba 2025. Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ,makosa 32 (asilimia 0.6 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa).


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Oktoba 2025**




Kosa kuu lililoripotiwa mwezi wa Oktoba 2025 ni kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (Makosa 2,354) yakifuatia kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (makosa 1,730).

Orodha ya makosa haya mawili (2) ya barabarani kati ya yote 10 yaliyoripotiwa mwezi Oktoba 2025 yamechangia asilimia 72.5


**Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani, Oktoba 2025**



Idadi ya makosa kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 15.0 na kufikia makosa 5,631 mwezi wa Oktoba 2025 kutoka makosa 6,627 mwezi wa Septemba 2025.

Wilaya ya Mjini imekuwa na idadi kubwa ya makosa ya barabarani kwa mwezi wa Oktoba 2025 (Makosa 1,262) ikilingalishwa na Makosa 1,204 yaliyoripotiwa mwezi wa Septemba 2025


**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Mwezi wa Oktoba 2025 na Septemba 2025**




Idadi ya makosa kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 6.9 na kufikia makosa 5,631 mwezi wa Oktoba 2025 kutoka makosa 5,268 mwezi wa Oktoba 2024.

Wilaya ya Mjini imekuwa na idadi kubwa ya makosa yaliyoripotiwa mwezi wa Oktoba 2025 (Makosa 1,262) ikilinganishwa na Wilaya ya Kaskazini 'B' ilikuwa na idadi kubwa ya makosa yaliyoripotiwa mwezi wa Oktoba 2024 (makosa 957)

**Kielelezo 2.3: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Mwezi wa Oktoba 2025 na Oktoba 2024**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi mbali mbali. Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabaraniza ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 31 zimeripotiwa mwezi Oktoba, 2025. Wilaya ya Kati imeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni sita (6) sawa na asilimia 19.4 ya ajali zote ikilinganishwa na wilaya nyengine.

Idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Oktoba, 2025 zilikuwa idadi sawa na ajali zilizoripotiwa mwezi wa Septemba 2025 (ajali 31)

Jumla ya makosa 5,631 yameripotiwa mwezi wa Oktoba 2025, ambapo makosa 5,629 yameripotiwa kwa wanaume na makosa 4 kwa wanawake.

Kosa kuu lililoripotiwa mwezi wa Oktoba 2025 ni Kutokufuuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 2,354) sawa na asilimia **41.8** ya makosa yote yaliyoripotiwa.

## Kiambatanisho:

**Jadweli 3.0: Idadi ya Ajali za Barabarani Zilizoripotiwa 2020-2025**

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 51 | 19 | 19 | 18 | 22 | 8 |
| Februari | 44 | 25 | 16 | 13 | 19 | 6 |
| Machi | 21 | 18 | 21 | 13 | 14 | 20 |
| Aprili | 22 | 20 | 9 | 15 | 18 | 27 |
| Mei | 30 | 18 | 16 | 12 | 20 | 14 |
| Juni | 21 | 14 | 5 | 12 | 23 | 24 |
| Julai | 20 | 19 | 14 | 24 | 21 | 25 |
| Agosti | 16 | 15 | 15 | 19 | 16 | 26 |
| Septemba | 11 | 10 | 14 | 16 | 16 | 31 |
| Oktoba | 23 | 19 | 11 | 16 | 19 | 31 |
| Novemba | 21 | 20 | 20 | 14 | 21 | |
| Disemba | 26 | 12 | 12 | 21 | 13 | |
| **Jumla** | **306** | **209** | **172** | **193** | **222** | **212** |

**Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani walioripotiwa 2020-2025**

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 89 | 44 | 36 | 38 | 40 | 10 |
| Februari | 76 | 40 | 29 | 19 | 49 | 8 |
| Machi | 40 | 31 | 60 | 16 | 27 | 48 |
| Aprili | 43 | 41 | 16 | 25 | 38 | 35 |
| Mei | 36 | 28 | 21 | 28 | 25 | 34 |
| Juni | 31 | 20 | 4 | 25 | 33 | 38 |
| Julai | 30 | 47 | 15 | 51 | 30 | 30 |
| Agosti | 41 | 37 | 48 | 65 | 32 | 65 |
| Septemba | 28 | 20 | 26 | 24 | 24 | 46 |
| Oktoba | 60 | 71 | 17 | 25 | 36 | 51 |
| Novemba | 44 | 45 | 28 | 26 | 54 | |
| Disemba | 34 | 20 | 23 | 43 | 25 | |
| **Jumla** | **552** | **444** | **323** | **385** | **413** | **365** |

### Jadweli 3.2: Idadi ya Waliofariki kwa Ajali za Barabarani Zilizoripotiwa 2020-2025

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 24 | 11 | 19 | 15 | 13 | 8 |
| Februari | 20 | 13 | 16 | 11 | 23 | 8 |
| Machi | 13 | 17 | 14 | 12 | 8 | 21 |
| Aprili | 10 | 18 | 6 | 12 | 13 | 22 |
| Mei | 13 | 14 | 10 | 6 | 14 | 15 |
| Juni | 20 | 11 | 4 | 10 | 17 | 17 |
| Julai | 12 | 13 | 12 | 16 | 17 | 22 |
| Agosti | 9 | 10 | 10 | 11 | 14 | 45 |
| Septemba | 6 | 11 | 13 | 13 | 17 | 21 |
| Oktoba | 16 | 21 | 8 | 14 | 16 | 32 |
| Novemba | 17 | 16 | 14 | 12 | 24 | |
| Disemba | 20 | 13 | 10 | 21 | 13 | |
| **Jumla** | **180** | **168** | **136** | **153** | **189** | **211** |

### Jadweli 3.3: Idadi ya Waliojeruhiwa kwa Ajali za Barabarani Zilizoripotiwa 2020-2025

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 65 | 33 | 17 | 23 | 27 | 2 |
| Februari | 56 | 27 | 13 | 8 | 26 | 0 |
| Machi | 27 | 14 | 46 | 4 | 19 | 27 |
| Aprili | 33 | 23 | 10 | 13 | 25 | 13 |
| Mei | 23 | 14 | 11 | 22 | 11 | 19 |
| Juni | 11 | 9 | 0 | 15 | 16 | 21 |
| Julai | 18 | 34 | 3 | 35 | 13 | 15 |
| Agosti | 32 | 27 | 38 | 54 | 18 | 20 |
| Septemba | 22 | 9 | 13 | 11 | 7 | 25 |
| Oktoba | 44 | 50 | 9 | 11 | 20 | 19 |
| Novemba | 27 | 29 | 14 | 14 | 30 | |
| Disemba | 14 | 7 | 13 | 22 | 12 | |
| **Jumla** | **372** | **276** | **187** | **232** | **224** | **161** |

**Jadweli 3.4: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Oktoba 2025.**

| Wilaya | Ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla ya Wathirika | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Idadi | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 5 | 16.1 | 4 | 2 | 6 | 18.8 | 0 | 1 | 1 | 5.3 | 4 | 3 | 7 | 13.7 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 9.7 | 2 | 0 | 2 | 6.3 | 1 | 0 | 1 | 5.3 | 3 | 0 | 3 | 5.9 |
| Kati | 6 | 19.4 | 4 | 1 | 5 | 15.6 | 3 | 0 | 3 | 15.8 | 7 | 1 | 8 | 15.7 |
| Kusini | 2 | 6.5 | 2 | 0 | 2 | 6.3 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 0 | 2 | 3.9 |
| Mjini | 1 | 3.2 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 5.3 | 1 | 0 | 1 | 2.0 |
| Magharibi 'A' | 5 | 16.1 | 6 | 0 | 6 | 18.8 | 2 | 0 | 2 | 10.5 | 8 | 0 | 8 | 15.7 |
| Magharibi 'B' | 3 | 9.7 | 3 | 0 | 3 | 9.4 | 1 | 0 | 1 | 5.3 | 4 | 0 | 4 | 7.8 |
| Wete | 3 | 9.7 | 3 | 0 | 3 | 9.4 | 8 | 0 | 8 | 42.1 | 11 | 0 | 11 | 21.6 |
| Micheweni | 1 | 3.2 | 1 | 0 | 1 | 3.1 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 2.0 |
| Chake chake | 1 | 3.2 | 1 | 1 | 2 | 6.3 | 0 | 2 | 2 | 10.5 | 1 | 3 | 4 | 7.8 |
| Mkoani | 1 | 3.2 | 1 | 1 | 2 | 6.3 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 1 | 2 | 3.9 |
| **Zanzibar** | **31** | **100** | **27** | **5** | **32** | **100** | **16** | **3** | **19** | **100** | **43** | **8** | **51** | **100** |

Jadweli 3.5: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Oktoba 2025

| Wilaya | Idadi ya Ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | | | Waendao kwa Miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Wa liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Wa liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 | 5 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 | 5 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Kusini | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| Magharibi 'B' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 3 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **31** | **3** | **0** | **3** | **0** | **0** | 0 | **6** | **3** | **9** | **10** | **3** | **13** | **12** | **2** | **14** | **4** | **0** | **4** | **6** | **0** | **6** | **2** | **0** | **2** |

## Jadweli 3.6: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya  Mwezi wa Oktoba 2025 na Septemba 2025

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** | **Sept-25** | **Okt-25** |
| Kaskazini 'A' | 2 | 5 | 2 | 1 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 3 | 10 | 1 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 4 | 6 | 0 | 3 | 4 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 5 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| Kusini | 4 | 2 | 5 | 0 | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini | 2 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 5 | 0 | 2 | 3 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 1 | 2 | 2 |
| Magharibi 'B' | 5 | 3 | 3 | 1 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Wete | 3 | 3 | 2 | 8 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 8 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Micheweni | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Chake chake | 2 | 1 | 2 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **31** | **31** | **25** | **19** | **21** | **32** | **0** | **0** | **2** | **3** | **17** | **13** | **4** | **9** | **7** | **4** | **8** | **14** | **1** | **2** | **7** | **6** |

**Jadweli 3.7: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi Oktoba 2024 na Oktoba 2025**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Walioathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 | Okt 2024 | Okt 2025 |
| Kaskazini 'A' | 8 | 5 | 16 | 1 | 4 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 | 1 | 2 | 5 | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 1 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 3 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 6 | 0 | 3 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini | 2 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 5 | 0 | 2 | 2 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 1 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 5 | 3 | 1 | 1 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Wete | 0 | 3 | 0 | 8 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Micheweni | 2 | 1 | 3 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **19** | **31** | **20** | **19** | **16** | **32** | **0** | **0** | **0** | **3** | **13** | **13** | **3** | **9** | **2** | **4** | **7** | **14** | **5** | **2** | **6** | **6** |

## Jadweli 3.8: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Oktoba 2025

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji Hatari | | | Ubovu wa Vipando | | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila yaleseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 43 | 0 | 43 | 227 | 0 | 227 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 | 17 | 286 | 0 | 286 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 75 | 0 | 75 | 90 | 0 | 90 | 15 | 0 | 15 | 110 | 0 | 110 | 126 | 0 | 126 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 40 | 0 | 40 | 0 | 0 | 0 | 400 | 0 | 400 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 43 | 0 | 43 | 150 | 0 | 150 | 239 | 0 | 239 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 39 | 0 | 39 | 70 | 0 | 70 | 214 | 0 | 214 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 27 | 0 | 27 | 34 | 0 | 34 | 170 | 0 | 170 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 31 | 0 | 31 | 9 | 0 | 9 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 6 | 0 | 6 | 17 | 0 | 17 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 20 | 0 | 20 | 30 | 2 | 32 | 23 | 0 | 23 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 15 | 0 | 15 | 20 | 0 | 20 | 19 | 0 | 19 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **0** | **82** | **0** | **82** | **103** | **0** | **103** | **205** | **0** | **205** | **511** | **2** | **513** | **1730** | **0** | **1730** |

**Inaendelea… Jadweli 3.8: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Oktoba 2025**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 35 | 0 | 35 | 331 | 0 | 331 | 2 | 0 | 2 | 646 | - | 646 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 54 | 0 | 54 | 453 | 0 | 453 | 1 | 0 | 1 | 811 | - | 811 |
| Kati | 60 | 0 | 60 | 40 | 0 | 40 | 85 | 0 | 85 | 98 | 0 | 98 | 30 | 0 | 30 | 729 | - | 729 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 60 | 0 | 60 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 510 | - | 510 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 66 | 0 | 66 | 764 | 0 | 764 | 0 | 0 | 0 | 1,262 | - | 1,262 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 80 | 0 | 80 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 403 | - | 403 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 56 | 0 | 56 | 0 | 0 | 0 | 660 | 0 | 660 | 0 | 0 | 0 | 947 | - | 947 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 40 | 0 | 40 | 19 | 0 | 19 | 0 | 0 | 0 | 101 | - | 101 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 32 | - | 32 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 0 | 25 | 19 | 0 | 19 | 0 | 0 | 0 | 118 | 2 | 120 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 70 | - | 70 |
| **Zanzibar** | **60** | **0** | **60** | **96** | **0** | **96** | **455** | **0** | **455** | **2,354** | **0** | **2,354** | **33** | **0** | **33** | **5,629** | **2** | **5,631** |

Jadweli 3.9: Idadi ya Makosa Barabarani, Baina ya Mwezi wa Oktoba, 2025 na Septemba, 2025

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 5 | 5 | 0 | 3 | 2 | 0 | 30 | 43 | 231 | 227 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 22 | 17 | 311 | 286 |
| Kati | 0 | 0 | 80 | 75 | 95 | 90 | 25 | 15 | 108 | 110 | 170 | 126 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 40 | 100 | 0 | 450 | 400 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 35 | 43 | 49 | 150 | 210 | 239 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 44 | 39 | 67 | 70 | 198 | 214 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 24 | 27 | 42 | 34 | 123 | 170 |
| Wete | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 24 | 31 | 9 | 9 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 4 | 11 | 6 | 26 | 17 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 20 | 20 | 19 | 32 | 24 | 23 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 14 | 15 | 9 | 20 | 14 | 19 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **87** | **82** | **95** | **103** | **167** | **205** | **481** | **513** | **1,766** | **1,730** |

Inaendelea... Jadweli 3.9: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Oktoba, 2025 na Septemba, 2025

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za Serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalamabarabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 | Septemba 2025 | Oktoba 2025 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 41 | 35 | 517 | 331 | 2 | 2 | 828 | 646 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 76 | 54 | 522 | 453 | 1 | 1 | 932 | 811 |
| Kati | 70 | 60 | 65 | 40 | 120 | 85 | 62 | 98 | 50 | 30 | 845 | 729 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 39 | 60 | 0 | 0 | 0 | 0 | 589 | 510 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 62 | 66 | 848 | 764 | 0 | 0 | 1204 | 1262 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 74 | 80 | 688 | 0 | 0 | 0 | 1071 | 403 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 56 | 52 | 0 | 670 | 660 | 0 | 0 | 911 | 947 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 | 40 | 17 | 19 | 0 | 0 | 69 | 101 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 5 | 0 | 0 | 45 | 32 |
| Chake chake | 14 | 0 | 0 | 0 | 8 | 25 | 5 | 19 | 0 | 0 | 90 | 120 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 10 | 3 | 5 | 0 | 0 | 43 | 70 |
| Zanzibar | **84** | **60** | **65** | **96** | **491** | **455** | **3,338** | **2,354** | **53** | **33** | **6,627** | **5,631** |

Jadweli 3.10: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Oktoba 2024 na Oktoba 2025

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 5 | 3 | 3 | 0 | 0 | 97 | 43 | 132 | 227 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 172 | 17 | 358 | 286 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 75 | 0 | 90 | 60 | 15 | 50 | 110 | 390 | 126 |
| Kusini | 0 | 0 | 54 | 0 | 40 | 10 | 60 | 40 | 102 | 0 | 141 | 400 |
| Mjini | 0 | 0 | 19 | 0 | 0 | 0 | 45 | 43 | 155 | 150 | 280 | 239 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 15 | 0 | 25 | 0 | 70 | 39 | 192 | 70 | 215 | 214 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 20 | 0 | 44 | 0 | 47 | 27 | 152 | 34 | 185 | 170 |
| Wete | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 2 | 33 | 31 | 19 | 9 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 4 | 19 | 6 | 34 | 17 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 34 | 20 | 34 | 32 | 54 | 23 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 20 | 15 | 17 | 20 | 29 | 19 |
| **Zanzibar** | **-** | **-** | **109** | **82** | **112** | **103** | **350** | **205** | **1,023** | **513** | **1,837** | **1,730** |


Inaendelea... **Jadweli 3.10: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Oktoba 2024 na Oktoba 2025**

| Wilaya | Kushindwa kuandika Anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za Serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 | Oktoba 2024 | Oktoba 2025 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 51 | 35 | 196 | 331 | 1 | 2 | 480 | 646 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 55 | 54 | 372 | 453 | 0 | 1 | 957 | 811 |
| Kati | 0 | 60 | 0 | 40 | 150 | 85 | 0 | 98 | 0 | 30 | 650 | 729 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 104 | 60 | 20 | 0 | 20 | 0 | 541 | 510 |
| Mjini | 35 | 0 | 25 | 0 | 175 | 66 | 85 | 764 | 0 | 0 | 819 | 1262 |
| Magharibi 'A' | 15 | 0 | 10 | 0 | 90 | 80 | 70 | 0 | 0 | 0 | 702 | 403 |
| Magharibi 'B' | 16 | 0 | 12 | 56 | 108 | 0 | 80 | 660 | 0 | 0 | 664 | 947 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 40 | 29 | 19 | 0 | 0 | 98 | 101 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 6 | 5 | 0 | 0 | 70 | 32 |
| Chake chake | 8 | 0 | 13 | 0 | 44 | 25 | 0 | 19 | 0 | 0 | 187 | 120 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 22 | 10 | 12 | 5 | 0 | 0 | 100 | 70 |
| **Zanzibar** | **74** | **60** | **60** | **96** | **812** | **455** | **870** | **2,354** | **21** | **33** | **5,268** | **5,631** |


**Jadweli 3.11: Tozo Zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya Kesi, Oktoba 2025**

| Wilaya | Idadi ya Kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 646 | 15,619,100 |
| Kaskazini 'B' | 811 | 19,608,500 |
| Kati | 729 | 25,141,625 |
| Kusini | 520 | 8,383,875 |
| Mjini | 1,262 | 31,425,300 |
| Magharibi 'A' | 1,180 | 29,389,750 |
| Magharibi 'B' | 947 | 25,168,350 |
| Wete | 101 | 1,690,500 |
| Micheweni | 32 | 736,000 |
| Chake chake | 120 | 2,139,000 |
| Mkoani | 81 | 1,434,500 |
| **Zanzibar** | **6,429** | **160,736,500** |

**Kielelezo1: Ajali za Barabarani Zilizoripotiwa kwa Wilaya, Oktoba, 2025**



**Kielelezo 2:Vifo na Majeruhi Wanaotokana na Ajali za Barabarani kwa Wilaya Oktoba, 2025**



## Zingatia Maelezo

Ajali ya barabarani inahusu ajali yeyote inayohusisha angalau gari moja barabarani, inayotokea barabarani kwa mzunguko wa umma na angalau mtu mmoja amekufa au amejeruhiwa. Kutokana na Sheriaya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar).

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumiagari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu.Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

### KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321,
Simu: +255242231869,
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com,
Nukushi: 024223136,
**MMP, Zanzibar**